**MASWALI NA MAJIBU WALIOITWA USAILI UCHAGUZI MKUU 2025**

## 1.Jina lako linafupi na utuambie kidogo kuhusu wewe

Jibu: Ninaitwa …, nina elimu ya …, na uzoefu wa kazi za usimamizi wa nyaraka. Mi mi ni makini, nina nidhamu na uwezo wa kushughulikia kazi kwa wakati

## 2.Kwa nini unataka nafasi ya Karani Msaidizi katika uchaguzi?

Jibu: Nataka kuchangia kuhakikisha uchaguzi hufanyika kwa haki na nina ujuzi wa us imamizi wa nyaraka na data unaohitajika.

## 3.Je, unafahamu majukumu ya Karani Msaidizi katika uchaguzi?

Jibu: Kusimamia kuandikishwa kwa wapiga kura, kukagua kadi za utambulisho, kuan daa nyaraka za uchaguzi, na kuhakikisha taratibu zinafuatwa kwa usahihi.

## 4. Una uzoefu wowote wa kazi zinazohusiana na usimami zi wa nyaraka, kuingiza data au utawala wa ofisini?

Jibu: Ndiyo, nimefanya kazi za kuandaa na kuhifadhi nyaraka, kuingiza data kwenye kompyuta na kupanga kumbukumbu kwa usahihi.

## 5.Je, umewahi kushughulikia mabadiliko au msongo wa kazi?

Jibu: Ndio, kwa kupanga vipaumbele, kusanifu ratiba na kushirikiana na wengine ili

k uhakikisha kazi inakamilika kwa wakati.

## 6.Ni hatua gani unazochukua kuhakikisha usahihi wa d ata na nyaraka zako?

Jibu: Kupitia mara mbili (double check), kutumia checklist, na kuhakikisha nakala za backup zinapatikana.

## 7.Je, una ujuzi wa matumizi ya kompyuta na programu  za ofisi?

Jibu: Ndio, ninaweza kutumia Word, Excel na PDF, na nina uwezo wa kujifunza prog ramu mpya haraka.

## 8.Unaweza kufanya kazi kwa muda mrefu au usiku s iku ya uchaguzi?

Jibu: Ndio, niko tayari kufanya kazi muda wowote inapohitajika kuhakikisha uchaguz i unakamilika vizuri.

## 9.

## Kwa nini tuchague wewe badala ya mtu mwingine?

Jibu: Mimi ni mwaminifu, nina nidhamu, nina ujuzi wa usimamizi wa nyaraka na nin a uwezo wa kufanya kazi bila usimamizi mkubwa.

## 10.Ni hali gani unaweza kukabiliana na migogoro au watu wasiokubali matokeo ya uchaguzi?

Jibu: Nitakaa mtulivu, kueleza taratibu kwa upole, na ikiwa hali ni ngumu nitaelekeza kwa msimamizi mwenye mamlaka.